TANGAZO LA SERIKALI Na. 399 ka Tarehe 16/6/2023

SHERIA YA USHURU WA STEMPU,
(SURA YA 189)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 16(1))*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA STEMPU YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii, itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Stempu ya mwaka 2023.

Tafsiri

2. Katika Amri hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"haki ya madini" maana yake ni leseni zinazorejewa katika kifungu cha 7 cha Sheria ya Madini;

"Makubaliano" maana yake ni Makubaliano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jacana Resources (Tanzania) Limited yaliyoingiwa tarehe 13 Desemba, 2021 ambapo Nyati Minerals Sands Limited iliundwa; na

"ushuru wa stempu" maana yake ni ushuru wa stempu unaotolewa kwa hati ambao ungeweza kutozwa chini ya kifungu cha 5(1) cha Sheria unaotokana na upangaji mpya wa hisa au umiliki wa hisa na uhamishaji wa haki za madini kutoka Jacana Resource (Tanzania) Limited kwenda kwa Nyati Minerals Sands Limited kwa mujibu wa Ibara ya 7.2(j) ya Makubaliano.

Msamaha

3. Ushuru wa stempu unaotokana na hati yoyote inayohusisha upangaji mpya wa hisa au umiliki wa hisa na uhamishaji wa haki za madini kutoka Jacana Resources (Tanzania) Limited kwenda Nyati Minerals Sands Limited, unasamehewa.

Ukomo

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo mara baada ya kukamilika kwa upangaji mpya na uhamishaji wa haki za madini zinazorejewa chini ya aya ya 3.

Dodoma,
2 Juni, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha na Mipango*